**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MTIHANI WA UTAMILIFU WA PAMOJA – KIDATO CHA NNE**
**(TANGA, IRINGA, SINGIDA, MOROGORO, DODOMA, TABORA, LINDI AND MTWARA)**

**021**

# KISWAHILI

(Kwa Watahiniwa wa Shule na wa Kujitegemea)

**Muda: Saa 3** **Mwaka: 2025**

---

## MAELEKEZO

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali **kumi na moja (11)**.
2. Jibu maswali yote katika sehemu A na B, na maswali **mawili (2)** kutoka sehemu C ambapo swali la **tisa (9)** ni la lazima.
3. Sehemu A ina alama **kumi na sita (16)**, sehemu B alama **hamsini na nne (54)** na sehemu C ina alama **thelathini (30)**.
4. Zingatia maelekezo ya **kila sehemu** na ya **kila swali**.
5. Vifaa vya mawasiliano na vitu visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

Mtihani huu una kurasa **4** zilizochapwa

## SEHEMU A: (ALAMA 10)

Jibu Maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Katika kipengele (i) - (x), chagua jibu sahihi kisha andika herufi ya jibu hilo kwenye kijitabu chako cha kujibia.

(i) "Kuku, wali nani?" Dhima ya muundo wa mazungumzo haya ni ipi?

A. Kupunguza ukali wa mazungumzo
B. Kufupisha urefu wa mazungumzo ( )
C. Kupamba lugha ya mazungumzo
D. Kuonyesha msisitizo wa mazungumzo
E. Kukidhi haja ya mazungumzo

(ii) Maneno yafuatayo yana maana zaidi ya moja isipokuwa:

A. Ua B. Mbuzi ( )
C. Kata D. Nyau
E. Paa

(iii) Mshororo wa mwisho ambao haubadiliki katika beti zote za utenzi huitwa:

A. Mshororo takriri B. Bahari ( )
C. Kituo bahari D. Kitulizo
E. Kituo

(iv) Tamathali ipi ya semi hukipa kitu kisicho binadamu sifa ya ubinadamu?

A. Taniaba B. Takiriri
C. Nidaa D. Tashihishi ( )
E. Tashibiha

(v) Mwalimu Juma aliwapa wanafunzi wake kamusi za Kiswahili kisha akawaambia wabainishe umuhimu wa kamusi katika lugha. Jifanye wewe ni miongoni mwa wanafunzi hao. Je ni umuhimu upi ambao hautapata katika kamusi?

A. Kujua maana ya maneno B. Kujua asili ya maneno
C. Kujua kategoria ya maneno D. Kujua aina ya sentensi
E. Kujua matamshi ya neno

(vi) Maneno yapi kati ya haya yafuatayo yameundwa kwa njia ya ufananisho?

A. Malapa, kuku, vuma B. Chemshabongo, jungukuu, mtutu
C. Katambuga, pikipiki, ufyagio D. Bongolala, nyau, chamcha ( )
E. Batamzinga, kifaru, kifuniko

(vii) Tamthiliya ambayo wahusika wake wakuu mwishoni huonesha kufanikiwa inaitwa:

A. Riwaya B. Ramsa
C. Mikondo D. Hadithi fupi ( )
E. Tanzia

(viii) Kimapokeo nomino inayojitokeza upande wa kiarifu inaitwa:

A. Sentensi B. Prediketa
C. Kiima D. Shamirisho ( )
E. Chagizo

(ix) Katika lugha ya Kiswahili kuna maumbo tofauti ambayo huwakilisha mofimu moja, maumbo hayo huitwa:

A. Alofoni
B. Mofimu
C. Alomofu
D. Mofu
E. Foni

( )

(x) Paka amelala **chini** ya meza. Neno lilokozwa limetumika kama:

A. Kiwakilishi
B. Kihusishi
C. Kiunganishi
D. Kielezi
E. Kivumishi

( )

2. Oanisha maneno yafuatayo toka **ORODHA A** kwenda **ORODHA B** kutoka katika mada ya fasihi simulizi, kisha andika herufi ya jibu sahihi katika kisanduku ulichopewa.

| ORODHA A | ORODHA B |
|---|---|
| (i) Hutumiwa kuonesha kuwa sentensi imekamilika. | A. Nukta |
| (ii) Hutumiwa kuonesha kuwa kuna orodha inafuata. | B. Ritifaa |
| (iii) Hutumiwa kwenye nukuu kuonesha kuwa kuna maneno ambayo yameachwa. | C. Nukta katishi |
| (iv) Hutumiwa kuweka pumziko fupi. | D. Mkato |
| (v) Hutumiwa kuonesha kuwa maneno yanayofuata au yanayotangulia yamesemwa au yametamkwa na msemaji mwengine. | E. Nukta pacha |
| (vi) Hutumiwa kuonesha kuwa neno limekatwa kwa kuwa limefika ukingoni mwa karatasi na bado linaendelea mstari unaofuata. | F. Alama za mtajo |
| | G. Nukta mkato |
| | H. Kistari |
| | I. Mkwaju |

## SEHEMU B: (ALAMA 54)

Jibu Maswali **yote** katika sehemu hii.

3. Kwa kutumia mifano anuai kutoka lugha ya Kiswahili, eleza maana ya istilahi zifuatazo kama zinavyotumika katika sarufi:
   (a) Silabi
   (b) Uambishaji
   (c) Mofimu tegemezi
   (d) Unyambulishaji
   (e) Mzizi
4. Fafanua nadharia tano zinazoeleza asili ya Kiswahili.
5. Kwa ufupi, eleza mambo sita (6) yanayotofautisha lugha ya mazungumzo na lugha ya maandishi.
6. (a) Wahusika wa fasihi simulizi wana upekee unaowapambanua, bainisha wahusika hao.
   (b) Eleza umuhimu wa kazi za fasihi simulizi kwa hoja tano.
7. (a) Kwa kutumia mifano, eleza vipashio vitano vya kiarifu.
   (b) Taja aina za sentensi unazozijua.

8. Soma shairi lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuata. Sema na wako msiri, mkiwa wawili ndani

Nje msiyahadhiri, yakawa ya hadharani Wawili mjisitiri, stara ina uzani
Kuweni na siri ndani, waume na wanawari
Si vyema kuyahubiri, mambo yenu mtaani Bure mtajiadhiri, watu watakusuteni
Ni muhimu kujisiri, muonwe bukheri shwari Kuweni na siri ndani, waume na wanawari
Mwisho wa langu shairi, nimefika ukingoni Nawaasa mkiri, mchunge yalo vichwani
Mipango msiabiri, iwe siri nyoyoni Kuweni na siri ndani, waume na wanawari.

**Maswali:**

(a) Nini dhamira ya shairi?
(b) Je, mshairi anatoa ujumbe gani?
(c) Je, shairi limetumika muundo gani?
(d) Andika msitari wa kituo bahari katika shairi hili.
(e) Mshairi ana maana gani asemapo "Kuweni na siri ndani, waume na wanawari"?
(f) Andika kina cha kati na cha mwisho katika shairi hili.

## SEHEMU C: (ALAMA 30)

Jibu maswali **mawili (2)** tu kutoka sehemu hii. Swali la **tisa (9)** ni la **lazima**.

### ORODHA YA VITABU

#### USHAIRI

| | | |
|---|---|---|
| **Wasakatonge** | – | M.S. Khatibu (DUP) |
| **Malenga Wapya** | – | TAKILUKI (DUP) |
| **Mashairi ya Chekacheka** | – | T.A. Mvungi (EP/D.LTD) |

#### RIWAYA

| | | |
|---|---|---|
| **Takadini** | – | Ben J. Hanson (MBS) |
| **Watoto wa Mama N'tilie** | – | E. Mbogo (H.P) |
| **Joka la Mdimu** | – | A.J. Safari (H.P) |

#### TAMTHILIYA

| | | |
|---|---|---|
| **Orodha** | – | Steve Reynolds (MA) |
| Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe | – | E. Semzaba (ESC) |
| **Kilio Chetu** | – | Medical Aid Foundation (TPH) |

9. Ni sifa zipi za fasihi simulizi zinazopotea mara fasihi hiyo inapoondolewa katika fasihi simulizi na kuwekwa katika maandishi.

10. Waandishi wa tamthiliya wamemchora mwanamke katika sura tofauti tofauti. Jadili kauli hii kwa kutumia vitabu viwili vya tamthiliya ulivyosoma.

11. Msanii wa kazi ya fasihi ni zao la jamii. Yote anayoyaandika katika kazi yake hutokana na jamii yake. Thibitisha usemi huu ukitumia vitabu viwili vya riwaya.